

ie muda huo kufanya  
kazi zenyet tija.

Alitoa rai hiyo wakati  
akizungumza na waandishi  
wa habari jijini hapa na  
kusema kuwa taifa linahitaji  
wananchi wake kuwajibika zaidi ili  
kujiepusha na mdoororo wa uchumi  
kwoo na kwa taifa.

Alisema kwenye kipindi  
di hiki ni sawa nchi kuwa  
katika vita na kama taifa  
sio wakati wa kulaumu  
serikali kupitia mitandao  
hiyo kwa kuwa haina tija.

Askopu mstaa fu huyo  
pia amewataka Watanzania  
kuendelea kumuomba  
Mungu kwa bidii na  
uaminifu ili ugonjwa huo  
uweze kupeku.

"Awali corona iliyovin-  
gia hapa nchini, tulifaniki-  
wa kwa kuomba huko  
tukifua maelekezo ya  
wataalamu wetu wa afya.

"Hivyo ni wakati pia  
hata kwa viongozi wa  
dini kuendelea kuhamasisha  
waumini ndani  
ya nyumba za ibada,  
moyo tuliokuwa nao  
huko nyuma wa kufanya  
maombi tuendelee kuwa  
nao," alisema.

Askopu huyo pia amewaomba  
Watanzania kuwajibika katika kuwaombe  
viongozi wa serikali ili  
Mungu aweze kuwa nao  
katika kuliogiza taifa.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega

Dodoma kumekuwa na ongezeko  
kubwa la watu na mahitaji ya maji  
yamekuwa yakiongezeka mradi  
huo una

Waziri huyo alisema awali

Dodoma kumekuwa na ongezeko  
kubwa la watu na mahitaji ya maji  
yamekuwa yakiongezeka mradi  
huo una

Pamoja na kuagiza fedha hizo

chico la Nzuzuni.

Pia unahusisha uendelezaji wa  
visima, ujenzi wa vibanda vyat  
kudeshea visima, ujenzi wa kibanda  
cha mlini na Chembu kwenye  
viungo muhimu vyat mabomba.

nuno ni utekelejaji  
kuboresha huduma

"Tumekabidhi n  
kati ya 850 za awan  
kuboresha huduma  
eneo hilo," alisema

Wakizungumza  
tofauti, wakazi wa  
kuru serikali kwa  
napata huduma y  
ilikuwa ni kero y

Mwenyekiti v  
Onas Kwanga, a  
maji lilisababish.  
familia kutokana  
mia muda mwini  
ya maji.

Naye Diwani v  
Ugogoni, Elizabeth  
anaamini kupitia i  
wa Ibwaga watapa  
mfupi za kuchimb  
wa visima vyat maj

## HABARI LEO UK 5 AGOST 31 \*Ulega aagiza msako machinjio bubu\*

Na Anastasia  
Anyimike

**N**AIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wataalamu wa wizara hiyo kufanya msako wa machinjio bubu ikiwa ni baada ya kutoa elimu kwa waduu umuhimu wa kutumia machinjio rasmi.

Ulega ameyasema hayo jijini hapa wakati alipofanya ziara ya kushtukiza kujionea maendeleo ya ukarabati wa machinjio ya Jiji la Dodoma kutokana na maelekezo 15 aliyyotaoa Julai 15, mwaka huu.

Katika maelekezo hayo, Ulega alitaka uongozi wa Machinjio ya Jiji la Dodoma uliokuwa ukililitaji Sh bilioni tatoo kufanya ukarabati kutumia mapato ya ndani yaliyokuwa yaitumika kulipana posho kufanya ukarabati awamu kwa awamu.

Alisema ni vyema wataalamu wakatoa elimu kubwa waduu kutumia machinjio na maeneo rasmi katika kuchakata ili kupata bidhaa zilizoandalia katika mazingira salama.

Alisema baada ya elimu kutolewa kitakachofuata ni kufanya operesheni maalumu na kwenda kuwaondosha wale wote wanaofanya kazi hizi kinyume na utaratibu.

"Tusingependa kuendelea kufanya kazi hizo kiholela holela, tunapaswa kuzingatia utaratibu ili kuwalinda walaji wapate kitu wanachotaka katika mazingira yaliyo bora na salama.

"Wasichinje huko vichakani na maeneo yasiyo rasmi, waje hapa machinjio yao ya serikali, bei ni nzuri na tuna wataalamu na mazingira yameboreshwa, wakiwa na changamoto yoyote katika huduma zinazotolewa wasifofu, watueleze na wizara itasikiliza na kuzitatua mara moja," alisema.

Pamoja na kuridhishwa na ukarabati unaoendelea ambapo hadi sasa Sh milioni 40 za mapato ya ndani zimetumika, Ulega alisitisita kuwa atahakikisha kila maelekezo anayoyatooa anayafutilia kwa karibu.

Awali, Kaimu Mkrugenzi wa Idara ya

Uzalishaji na Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Michael, alisema kwa Julai na Agosti mapato yameshuka kutokana na baadhi ya wafanyakishara wengi kuanza kuchinja mifugo maporini au katika mae-neo yasiyo rasmi.

Alisema katika kipindi cha Agosti 26 mwaka huu, machinjio yamekusanya Sh milioni 54.287 kutoka kwenye biashara ya uchinjaji wa mifugo pamoja na mapato mengine ukiliganisha na makusanyo ya Julai tarehe kama hiyo ambapo ilikuwa Sh milioni 72.093 na hivyo kushuka kwa asilimia 33.

Michael alisema katika kipindi cha Agosti mosi hadi 26 mwaka huu, jumla ya ng'ombe 2,844 walichinjwa kwa ajili ya soko la ndani na ng'ombe 38 walichinjwa kwa ajili ya soko la nje.

Pia alisema mbuzi na kondoo 17 walichinjwa kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi za Qatar na Kuwait.

"Katika kipindi cha Julai na Agosti wastani wa ng'ombe walioletwa kwa ajili ya soko la ndani umeshuka kutoka 130 hadi 90 kwa siku, hii inashiria kwamba wafanyakishara wengi wameanza kuchinja mifugo maporini au katika mae-neo yasiyo rasmi na

hii itahatarisha afya za walaji wa nyama katika Jiji la Dodoma," alisema Michael.

Akizungumzia ukarabati wa machinjio hayo, Michael alisema hadi ku-fikia Agosti 26, ukarabati umefikia zaidi ya asilimia 90 ambapo zaidi ya Sh bilioni 40.094 zimetumika katika kazi hiyo.

**SHUKRANI**



Familia ya marehemu Danford Nelson Mbilinyi wa M Salaam, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa makundi i wote waliotukimbia na kutufarji katika wakati mg kuondokewe na Mpewda wetu, Baba wa familia Dan aliyefariki tarehe 28/7/2021 na mazishi tarehe 31/7/2021 Mkoani Iringa.

Kipekee kabisa, tunashukuru Uongozi wa KKKT Dayo ikiba ni pamoja Mkuu wa Jimbo la Pomerini, Mchungaji Lukani na Washarka, Uongozi wa KKKT Dayosi ya Mash Uongozi wa KKKT (DMP) - Ushirika wa Makongo na Was TAG Antokia - Makongo Juu na CCT - U

Shukrani za pekee kabisa kwa Uongozi wa Umoja Sv zinazohirikiana na Umoja Switch Ltd, UBX, Mabenki ya Umoja Switch, Wanachama wa Tanzania Bankers As Rais, Sekretarieti ya Ajira katika utumishi wa Umma, Tos Association, Chama cha Mapinduzi Mkoaa wa Iringa, Yetu E Staff, Wanakijji wa Lukani- Kilolo Iringa, Majlirani Makong na Miganga West Dodoma, Ndugu, Jamia na

Kwa kuna si rahisi kutaja kila mmoja Japo tunatamani kunaomba kila mtu kwa upekee wake apokee shukra

**BWANA ALITOQIA, BWANA AMETWAA, JINA LAKE**

# \* Ulega aagiza kasi ukarabati machinjio

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvubi, Abdallah Ulega, ameagiza uongozi wa machinjio ya Jiji la Dodoma kuhakikisha unakamilisha ukarabati ifikapo Septemba 15, mwaka huu.

Agizo hilo aliltoa jana alipofanya ziara ya kushtukiza kujionea maendeleo ya ukarabati wa machinjio hayo ulioanza Julai 15, mwaka huu.

Ulega alisema ameridhishwa na ukarabati unoaoendelea kufanya ambapo hadi sasa zimetumika Sh. milioni 40 kwa kutumia mapato yake ya ndani.

"Kila maelekezo tunayoyatoa, tunayatoa kwa wakati maalum na kinachofuata ni ufuatiliaji wa karibu, tunatoa maelekezo na kufuatilia utekelezaji wake, tunawapongeza watendaji wetu wizarani maana kila maelekezo tunayoyatoa wanayamamia na mna fanya kazi nzuri maelekezo tunayoyatoa mnayafanya kazi," alisema.

Alisema anataka kuona machinjio hayo yanabadilika na kuwa bora.

"Nimeridhika na ukarabati unoaoendelea hadi sasa ambapo awali uongozi wa machinjio ulihitaji Sh. bilioni tatu, lakini niliagiza kuanza kufanya ukarabati kwa kutumia mapato ya ndani."

"Nilipotoa maelekezo nilitaka yanasmamiwe usiku na mchana na kuyafuatilia hadi mwisho wake nataka maboresho haya yawe yamekamilika kufikia Septemba 15, mwaka huu," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Mkrugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvubi, Stephen Michael, alisema hadi sasa ukarabati wa machinjio ya Jiji la Dodoma yamefikia zaidi ya asilimia 90 ambapo maeneo 13 kati ya 15 yatakuwa yamekamilika mwisho wa mwezi huu na maeneo mawili yaliyobakia yatakamilika Septemba 15, mwaka huu.

Alisema wamesimamia maelekezo hayo kutokana na kutambua athari zinazoweza kujitokeza kwa ulaji wa nyama isiyio na usalama.

# W ya

Na August

# M

jiji kusima  
kuwachuk  
hujumu n  
hiyo.

Emmar  
alipokuwa  
kusafirish  
ajili ya m  
na Mamla  
wa Mazin  
katika Kij  
humo.

Alisem



Mhand  
wataka  
juzi. PI

# Mradi wa eli

Fedha za ndani zilizotumika kwa ajili ya ukarabati

# \* Ulega akoleza moto machinjio ya Dodoma

Na MWANDISHI WETU

**N**AIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema atahakikisha anafruutilia kwa karibu maelezo yote anayotoa ili kujiridhisha na utekelezaji wake na kufikiwa kwa malengo ya Serikali.

Hayo aliyasema hayo juzi, alipofanya ziara ya kushtukiza kujionea maendeleo ya ukarabati wa machinjio ya Jiji la Dodoma yaliyoanza Julai 15, mwaka huu.

Ulega alieleza kuridhishwa na ukarabati unaondelea kufanywa, ambapo hadi sasa zimetumika sh.

millioni 40 kwa kutumia mapato ya ndani ya machinjio hayo.

"Kila maelekezo tunayoyatoa, tunayatoa kwa wakati maalumu na kinachofuata ni ufuutiliaji wa karibu, tunatoa maelekezo na kufuutilia utekelezaji wake

"Tunawapongeza watendaji wetu wizarani maana kila maelekezo tunayoyatoa wanayasimamia na mnafanya kazi nzuri maelekezo tunayotoa mnayafanya kazi," alisema.

Ulega alisema alitoa maelekezo ya machinjio ya jiji la Dodoma, kubadilika na kuwa bora, hivyo ameridhika na ukarabati unaoendelea hadi sasa, ambapo awali uongozi wa machinjio

ulihitaji sh. bilioni tatu, lakini aliwaelekeza kuanza kufanya ukarabati kwa kutumia mapato ya ndani.

Alisema yeye kama kiongozi anatoa maelekezo na kuhakikisha yanasisimamiwa usiku na mchana na kuyafuatilia hadi mwisho wake na kutaka maboresho hayo yawe yamekamilika kufikia Septemba 15, mwaka huu.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Masoko kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Michael, alisema ukarabati wa machinjio ya Jiji la Dodoma yamefikia zaidi ya asilimia 90.

Alisema maeneo 13 kati ya 15 yatakuwa yamekamilika mwisho wa mwezi huu na maeneo mawili yaliyobaki yatakamilika ifikapo Septemba 15, mwaka huu.

Michael alisema watendaji wanaposimamia maelekezo ya viongozi ni muhimu kwa kuwa wanajua athari zinazojitokeza kutoptana na ulaji wa nyama isiyokuwa usalama.

KAMATI YA UONGOZI

# \*Wizi wa mifugo watikisa Kagera\*

BUKOBA

NA MEDDY MULISA

**P**olis i mkoani Kagera inawashikilia watu wawili kwa tuhuma za wizi wa ng'ombe wanane wenyewe thamani ya Sh milioni 12.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Maketi Msangi, ameliambia JAMHURI kuwa ng'ombe hao ni mali ya Speratus Mbeikwa, mkazi wa Kijiji cha Kabale, Bukoba.

Anasema wizi huo ulitokea Agosti 21, mwaka huu ambapo Jeshi la Polisi, baada ya kupata taarifa, lilianzisha msako mkali na kufanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao.

"Watuhumiwa hao ni Anchilus Mwesiga (21), mlinzi wa Kampuni ya Nyamiaga, aliyekutwa na ng'ombe wanne aliowaficha katika Kijiji cha Itahwa. "Wa pili ni Shaidu Juma (31), mkazi wa Kijiji

cha Muhutwe, Muleba ambaye alikamatwa akiwa na ng'ombe watatu akitafuta mteja wa kumuuzia," anasema Msangi na kuongeza:

"Baada ya upelelezi kukamilika, watuhumiwa hawa watafikishwa mahakamani kujibu."

Wakati polisi wakiendelea na upelelezi wa tukio hilo, Diwani wa Ibwera, Michael Lubisi, ameliambia gazeti hili kwa njia ya simu kuwa takriban ng'ombe 29 waliibwa na watu wasiofahamika ndani ya miezi minne iliyopita.

Matukio hayo yametokea mfululizo katika vijiji vya Itongo na Kibona ambapo matukio mawili yalifanyika Itongo yakihuisha wizi wa ng'ombe 20.

Matukio mengine mawili yalifanyika katika Kijiji cha Kibona ambako ng'ombe wanne wa masista wa Shirika la Batheleza waliibwa huku mkazi wa kijijini hapo, Vincent Gamba, akiibiwa ng'ombe watano.

Matukio hayo yaliripotiwa Kituo cha Polisi cha Katoro, Halmashauri ya Bukoba.

Baadhi ya wadau wamesema ng'ombe wengi wanaoibwa vijiji husafirishwa na kuuzwa kinyemela katika machinjio ya Manispaa ya Bukoba.

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawiro, miezi michache iliyopita alitoa agizo la kuzuia mifugo kusafirishwa baada ya saa 12 jioni. Agizo hilo linaendelea.

Mmoja wa wafanyabiashara katika machinjio ya Manispaa ya Bukoba, Johari Hashim, anasema ulinzi umeimarishwa eneo hilo kwa kuweka uzio ambapo ng'ombe huwekwa wakisubiri kuchinjwa.

Wiki chache zilizopita, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alifanya ziara mkoani Kagera ambapo pia alitembelea machinjio hayo kuzungumza na wafanyabiashara wa mifugo.

Hata hivyo, Ndaki alieleza kutoridhishwa na hali ya machinjio hayo ambapo alimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba, Maurice Limbe, kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa machinjio hayo.

with rock pieces which he took for processing yielding significant quantity of gold.

village started spewing out gold the government moved in and held talks with people who owned the land in

Charles Mabeho.

"Personally I am very happy graced with the mineral among my

backyard, saying this provided opportunities for the development of the district.

THE GUARDIAN Page 4

AGOST 31, 2021.

## Minister wants revamping of Dodoma abattoir completed

By Guardian Reporter, Dodoma

LIVESTOCK and Fisheries Deputy Minister Abdallah Ulega has instructed top officials of the Dodoma City abattoir to make sure its revamping is completed by September 15 this year.

Ulega issued the directives here yesterday during his impromptu

visit at the abattoir to witness renovation work that began July 17 this year.

He said he was satisfied with the work ongoing saying so far 40m/- has been spent from the city council's internal sources.

"We praise our officials in the ministry as they oversee every directive we give, you are doing a

good job," he said, and added that he would like to see the abattoir changes for the better.

"When I gave the directives, I wanted them to be implemented day and night and I would like the work to be completed by September 15 this year," he added.

For his part, the ministry's Acting Director of Production and

Marketing, Stephen Michael said so far the renovation work has reached 90 per cent whereas 13 out of 13 areas have been completed and the remaining two will be completed by September 15 this year.

He said they have implemented the directives in recognition of adverse effects to consumers of unsafe meat.

reached among some discussants of entrepreneurship at

neighbouring countries.

The formation of the Tanzania Revenue Authority (TRA)

business, no markets.  
Change ca

# \*THE GUARDIAN Page 11 Govt, cooperative society launch 'school milk programme' in Hai

By Correspondent James Lanka, Hai

THE government in collaboration with the Nronga Women Dairy Cooperative Society (NWDS) has launched phase two of the 'School Milk Programme' in Hai District, Kilimanjaro Region reviving milk feeding initiative in the area.

During the inauguration ceremony over the weekend, several pupils from all primary schools within Hai District Council and other stakeholders gathered to celebrate the special event at Snow View grounds in Bomang'ombe town with the theme—"One glass of milk per day at least twice a week for better health and education".

The event was graced by the acting Permanent Secretary of the Ministry of Livestock and Fisheries (Livestock) Dr Asimwe Rweguza, Chairman of Hai District Council Edmund Lutaraka, Program Director for Heifer International, Mark Tsoxo and the Hai District Commissioner Juma Irando, among many dignitaries.

Speaking during the event, Tanzania Dairy Board (TDB) Registrar, Dr George Msalya said the launch of the program was vital as it helps in raising awareness among pupils' and the general public on the importance of consuming milk on daily basis.

He said while the World Health Organisation (WHO) recommends milk for better health, an individual is supposed to consume at least 200 litres of milk in a year, seeing a Tanzanian consumption currently at 54 litters annually being low.

He said that the TDB's decision to revive the school milk feeding pro-

gramme is aimed to improve milk consumption culture in Tanzania.

"Revival and improvement of school milk feeding programme will automatically push a fresh 'Milk Generation'," Msalya said.

During the event, government high rank officials and other dignitaries organized a special demonstration on milk drinking and awareness speeches, as well as free distribution of bottles of milk to the participants.

The Registrar further applauded the role played the Nronga Women Dairy Cooperative Society in the improving of milk sector in the country, noting that TDB was working around the clock to ensure that milk production in the country improves and consumption is also increased.

"Currently, milk production per year in Tanzania is 3.4 billion litres that is low and doesn't keep pace with the actual demand, and we have a deficit of 9 billion litres per year, and we do imports a total of 5 billion litres of milk from abroad per year," Dr. Msalya explained.

Statistics show that in 2017/18, Tanzania imported 20,920,537.58LME's Kg, valued at 30,290,485,222/- and 2018/19 the country imported LME's Kg 617,769 worth at 27, 961,44 due to low production of milk within the country.

Executive secretary of Nronga Women Dairy Cooperative Society (NWDS), Hellen Ussiri said they are facing several challenges including lack of title deed of the land where their dairy plant is located.

"The NWDCS factory is not centrally located to the market for their products. The land on which